

# TAHADHARI



Ikiwa unapokea chanjo katika duka hili la dawa au kliniki hii, maelezo yako ya chanjo yanaweza kutumwa kwa Mfumo wa Taarifa za Chanjo wa New Hampshire

## NHIS ni nini?

Mfumo wa Taarifa za Chanjo wa New Hampshire (NHIS) ni mfumo wa mtandao unaotii HIPAA ulioundwa na Kitengo cha Huduma za Afya ya Umma cha NH (DPHS). NHIS ni njia isiyolipishwa, iliyo salama, na rahisi ya kusasisha rekodi za chanjo bila kujali mahali ambapo chanjo inatolewa. New Hampshire ni jimbo la 50 katika taifa kupitisha sajili ya chanjo.

## Hii inaniathiri vipi?

- Taarifa zako zitatumwa kiotomatiki kwa NHIS kutoka kwa ofisi ya mtoa huduma wako, duka lako la dawa, au kliniki yako ukichagua kushiriki.
- Rekodi yako ya chanjo itahifadhiwa kwa usalama ili wewe na mtoa huduma wako muweze kuiona inapohitajika.
- Unaweza kupakua nakala ya rekodi zako au za mtoto wako kwa ajili ya shule, utunzaji wa watoto, au kambi za kiangazi.

## Ni taarifa gani inariyopotywa kwa NHIS?

- Taarifa za kimsingi kama vile jina, anwani, nambari ya simu, na barua pepe.
- Taarifa za kidemografia kama vile jinsia, rangi, na kabila.
- Taarifa za chanjo kama vile aina ya chanjo, nambari ya kundi, tarehe ya mwisho wa matumizi, na tarehe iliyotolewa.

## Jinsi ya kushiriki/Kutoshiriki:

- Una haki ya kuchagua kushiriki au kutoshiriki katika kuwasilisha taarifa zako kwa NHIS kwa kumjulisha mtoa huduma anayesimamia. Unaweza kuulizwa kujaza fomu inayoonyesha chaguo lako.
- Ukichagua kushiriki, utaombwa kutoa idhini ya wazi ya kuwasilisha taarifa zako/za mtoto wako na taarifa zako/za mtoto wako za chanjo zitaingizwa kwenye NHIS.
- Ukichagua kutoshiriki, taarifa zako hazitaingizwa kwenye NHIS.

